# RASIMU - 18/3/21

## Mpango wa Eneo kwa Mwaka 2021-2025 wa Idara ya Huduma kwa Watu Wazee, Walemavu na Wanajeshi Wastaafu

Idara ya Huduma kwa Watu Wazee, Walemavu na Wanajeshi Wastaafu (ADVSD) inatoa muhtasari ufuatao wa rasimu za malengo na maazimio ya Wakala wa Eneo kuhusu Mpango wa Eneo kuhusu Kuzeeka kwa Mwaka 2021-2025.

**Wazee wa Kabila Asili la Amerika**

1. Kuwahudumia wazee wa Makabila Asili ya Amerika wanaoishi katika maeneo ya mjini kwa kuunga mkono wakala zinazowahudumia.
    a. Vipaumbele vya Wazee wa kabila asili, vinavyohusiana na huduma na ustawi, na pia vya familia, makabila na jamii za makabila, vimeeleweka na kuangaziwa na ADVSD.
    b. Wazee wa makabila asili ya Amerika wanatumia mipango na huduma zinazofadhiliwa na ADVSD.

**Watu Wazima Wazee zaidi Waliobadilisha Jinsia na Wasio wa Mojawapo wa Jinsia Yoyote Kuu na Wazee wa Roho Mbili**

1. Watu Wazima Wazee zaidi Waliobadilisha Jinsia na Wasio wa Mojawapo wa Jinsia Yoyote Kuu na Wazee wa Roho Mbili wanashughulikiwa vizuri na jamii inayowajali na wanatumia huduma na miradi ya kuwezesha ustawi wao, uhuru na uwezo wa kujitawala.
    a. Kuongeza idadi ya watu wazima wazee zaidi Waliobadilisha Jinsia na Wasio wa Mojawapo wa Jinsia Yoyote Kuu na Wazee wa Roho Mbili wanaotafuta na kufikia huduma kutoka ADVSD na mtandao wa huduma kwa wazee.

2. Watu wazima wazee zaidi waliobadilisha Jinsia na wasio wa mojawapo wa jinsia yoyote kuu na Wazee wa Roho Mbili wanafanya mchakato wa kijamii wa kufikia huduma za watu wazee na watu wanaoishi na umemavu.
    b. Watu wazima wazee zaidi waliobadilisha Jinsia na wasio wa mojawapo wa jinsia yoyote kuu na Wazee wa Roho Mbili wanatambua, kuweka vipaumbele na kutoa mapendekezo yanayohusiana na mahitaji yao ya utoaji huduma za nyumbani na kijamii.

**Maelezo na Usaidizi (I &A) na Muunganisho wa Rasilimali za Wazee na Watu Wanaoishi na ulemavu (ADRC)**

1. Wazee, watu wanaoishi na ulemavu, na walezi wao wanatambua na kutumia ADRC kama nyenzo ya kufikia maelezo, rasilimali, na huduma.
    a. Kuongeza matumizi ya ADRC ili kupunguza kutengwa na vizuizi vya ufikiaji dhidi ya watu wazee waliotengwa kimwili, kitamaduni au kilugha.

2. Wazee, watu wanaoishi na ulemavu, familia zao na walezi wana uwezo wa kufikia rasilimali na huduma kupitia mtandao wa maelezo, rufaa na usaidizi.
    a. Washirika wa Jamii na mashirika yenye uhusiano na jamii kuhusu watu waliotengwa kihistoria na kimfumo wanajua na kutumia ADRC na mtandao wa I & A.

**Huduma za Lishe**

1. Wazee watapata chakula cha kutosha kwa cha bei nafuu, kinawachofaa kitamaduni, na kinachodumisha afya zao.
    a. Kuongeza matumizi ya mipango ya lishe inayofadhiliwa na serikali, kama vile Mpango wa Msaada wa Lishe ya Ziada au SNAP, jambo linalofanywa na wazee wengine
    b. Kuwezesha ufikiaji wa chakula cha bei nafuu au bila malipo katika mazingira mbalimbali ili kukidhi mahitaji mbalimbali ya wazee.

2. Kuunga mkono juhudi zinazoongozwa na jamii ili kuboresha ufikiaji wa chakula kwa wazee na watu wenye ulemavu, huku watu wenye waotengwa kihistoria na kimfumo wakipewa kipaumbele.
    a. Ufikiaji wa chakula na rasilimali za lishe zinapewa kipaumbele kwa watu wazima wazee waliotengwa kihistoria na kimfumo.

**Kudumisha Afya**

1. Wazee na watu wanaoishi na ulemavu wamewezeshwa kuwa na uhusiano thabiti katika jamii yao kuwezeshwa kustawi katika afya ya kimwili na kiakili.
    a. Kuogeza upatikanaji wa mafunzo na shughuli za kukuza afya kwa watu wazima kupitia ushirikiano na ukuzaji wa kimtandao.

2. Wazee wanashiriki kikamilifu katika shughuli za kukuza afya kushughulikia hali mbaya, kuboresha afya, na kupunguza kujitenga kwa watu.
    a. Watu wazima zaidi wanashiriki katika shughuli za kuboresha afya na ustawi wao.

**Watunzaji wa Familia**

1. Kukuza rasilimali na huduma za watunzaji wa familia kwa watunzaji wa familia na watunzaji wasio rasmi kuweka kipaumbele huduma kwa jamii zilizotengwa kihistoria na kimfumo.
    a. Kukuza ushiriki wa watunzaji wa familia na watunzaji wasio rasmi kuweka kipaumbele huduma kwa watunzaji kutoka kwa jamii zilizotengwa kihistoria na kimfumo.

2. Watunzaji wa familia wanapokea huduma za kibinafsi na za zinazowafaa kitamaduni.
    a. Kuongeza idadi ya watunzaji wa familia ambao wanapata huduma zinazofaa kitamaduni na zinazofanikiwa.

**Haki za Wazee na Usaidizi wa Kisheria**

1. Wazee wanapata ushauri wa kisheria kupitia Mradi wa Senior Law Project huku msisitizo ukiwa kuhusu ufikiaji zaidi kwa jamii zilizotengwa kihistoria na kimfumo.
    a. Usaidizi wa kisheria unatolewa kwa wastani wa watu wazima 900 kila mwaka.
    b. Kuongeza uwezo wa kuwahudumia wazee waliotengwa kihistoria na kimfumo kupitia Mradi wa Senior Law Project.

2. Wazee wana rasilimali za kijamii za kuwezesha watu kusaidiana na kujitetea miongoni mwa washirika.
    a. Kuandaa mpango wa ufikiaji ili kukuza rasilimali zilizopo za kujitetea na mitandao ya washirika.

**Usimamizi na Rasilimali za Usafiri**

1. Wazee wanaelewa rasilimali za usafiri zinazopatikana kwa ajili yao.
    a. Rasilimali za usafiri zinasambazwa kwa watu wazima wenye mahitaji makubwa, huku wanajamii waliotengwa kihistoria na kimfumo wakipewa kipaumbele.
    b. Rasilimali za usafiri zinaratibiwa katika mfumo wa huduma ya wazee.

2. Rasilimali za usafiri zinaupa kipaumbele upendeleo wa jamii na kufuata itifaki za usalama dhidi ya korona.
    a. Mahitaji yanayohusiana na usafiri na mapendeleo ya wazee yanayohusiana na utoaji wa huduma unaoendelea na janga la COVID-19 unaeleweka na kushughulikiwa na ADVSD.